



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI AJIRA ZA MUDA ZA MAKARANI NA WASIMAMIZI WA SENSA YA WATU NA MAKAZI KWA MWAKA 2022

UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko kwenye maandalizi ya kufanya Sensa ya Watu na Makazi ambayo itafanyika tarehe 23 Agosti 2022. Ili kufanikisha Sensa hii, Serikali ilitangaza nafasi za kazi za muda za **MAKARANI NA WASIMAMIZI WA SENSA** kwa Watanzania wenye nia na sifa zinazostahili kama ilivyoainishwa katika tangazo husika. Maombi ya kazi yalitakiwa kuwasilishwa kuanzia tarehe 05-19/05/2022. Aidha kazi zilizotangazwa katika tangazo husika ni:

1. **KARANI WA SENSA**
2. **MSIMAMIZI WA TEHAMA**
3. **MSIMAMIZI WA MAUDHUI**

Hivyo unajulishwa kuwa baada ya uchambuzi wewe ni mmojawapo/miongoni mwa wanaotakiwa kuhudhuria kwenye usaili katika maeneo yaliyoainishwa kulingana na nafasi uliyooomba

1.USAILI KWA KAZI ZA **KARANI WA SENSA NA MSIMAMIZI WA MAUDHUI** UTAFAANYIKA KATIKA KATA ULIOOMBEA KAZI KUANZIA TAREHE 19-21/07/2022 KAMA INAVYOONEKANA KWENYE ORODHA AMBAYO IMEAMBATANISHWA PAMOJA NA TANGAZO HILI

2.KWA WAOMBAJI WA KAZI YA **MSIMAMIZI WA TEHAMA** USAILI UTAFAANYIKA MAKAO MAKUU YA WILAYA KUANZIA TAREHE 19-21/07/2022

Kwa tangazo hili unatakiwa kufika katika eneo husika tayari kwa usaili siku ya jumanne tarehe 19/7/2022 na zoezi hili litanza mapema saa 3:00 asubuhi

Hakikisha unakuja na nyaraka muhimu zilizokuwa zimeainishwa kama hitaji mojawapo wakati wa maombi

Nakutakia maandalizi mema

“SENSA KWA MAENDELEO, JIANDAE KUHESEBIWA”

